

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI-MTWARA**



TANGAZO LA KAZI YA UFUNDI UJENZI

Tarehe 27/09/2018

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imepokea fedha kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa- TAMISEMI kwa ajili ya Ujenzi wa kituo cha afya **Chiungutwa**.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anatangaza nafasi ya kazi ya **FUNDI UJENZI** kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha Chiungutwa.

Majengo yatakayojengwa ni kama yafuatavyo:

1. Jengo la wagonjwa(OPD).
2. Wodi ya kulaza Wagonjwa.
3. Jengo la Mama na Mtoto.
4. Kichomea taka.
5. Shimo la kutupia kondo la nyuma.

Hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anakaribisha maombi ya mafundi ujenzi binafsi au vikundi vya fundi ujenzi wa majengo wenye/mwenye sifa zifuatazo:-

- i. Awe raia wa Tanzania.
- ii. Awe tayari kuheshimu mkataba wa kazi atakayopewa.
- iii. Awe na busara ya kusikiliza ushauri wa kitaalamu wa ujezi.
- iv. Awe anajua kusoma ramani /michoro na kutoa tafsiri sahihi.
- v. Awe na akaunti ya benki kwa ajili ya malipo.
- vi. Awe na mafundi wasaidizi, vibarua na vifaa vya kutosha.
- vii. Fundi awe na uwezo wa kujenga,kumaliza na kukabidhi kazi kwa muda waa miezi mitatu tu.
- viii. Nyaraka ya zabuni(Fomu za Maombi) zinapatikana katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni (Afisa Manunuzi) Hlmashauri ya Wilaya Masasi.
- ix. Maombi yote yawasilishwe ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni (Afisa Manunuzi) Masasi.
- x. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyo kamilika, maombi ambayo hayatakuwepo siku ya ufunguzi,hayatapokelewa na kuhusishwa na zoezi la uchambuzi wa kumpata fundi atakayefanya kazi ya ujenzi.
- xi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **11/10/2018 Saa 04:30** Asubuhi.
- xii. Maombi ya Zabuni yatafunguliwa tarehe **11/10/2018 Saa 04:30** Asubuhi

Ryoba E Magabe,
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA (W) MASASI.